# MUDA WA MABADILIKO: KUANZA SHULE VIZURI

## Mwongozo wa kusaidia familia kukamilisha *Transition Learning and Development Statement*

### KWA NINI NI MUHIMU KUANZA SHULE VIZURI?

Kuanza shule vizuri huleta matokeo mazuri zaidi kwa mtoto wako kama kujifunza vizuri zaidi na kutulia vizuri zaidi anapopitia mabadiliko mwanzoni na baadaye. Kuhakikisha mabadiliko yanayofaa na mazuri pia husaidia elimu na maendeleo ya mtoto wako kuendelea kwa mfululizo ; Kuweka mkazo mkubwa kwenye mwendelezo wa kujifunza inatambua kuwa kujenga juu ya uzoefu wa awali na sasa, huwasaidia mtoto wako kujihisi anatunzwa, kutohisi wasiwasi na kuwazoea watu wapya, mahali papya, matukio, utaratibu pamoja na kujua yanayotokea. Kuanza shule vizuri husababisha vijana kuimaraka.

### *TRANSITION LEARNING AND DEVELOPMENT STATEMENT* NI NINI?

Huduma zinazowatunza watoto wachanga, shule, huduma za *Outside School Hours Care (OSHC)* (Utunzaji wa Muda Nje ya Masaa ya Vipindi) pamoja na familia ni pamoja katika kulea elimu na furaha ya watoto. Ili kurahisisha ushirikiano wa maelezo kati ya huduma, shule na familia, kila mtoto anayo Transition Learning and Development Statement (Taarifa ya Mpito) ya kwake ambayo hutungwa na huduma ya watoto wadogo kwa kila mtoto anapotazamia kwenda shuleni.

Taarifa ya Mpito h*u*shirikisha maelezo kuhusu elimu ya mtoto wako, maendeleo na raha yake, baina ya huduma za watoto wadogo na shule. Taarifa ya Mpito hiyo inatoa taarifa kwa kifupi kuhusu shauku, vipawa na uwezo wa mtoto wako na inaonesha njia na mikakati (maarifa) hasa kwa mtoto wako ili kumsaidia anapojifunza.

Taarifa ya Mpito inaweza kukusaidia kufahamu, kutegemeza, kupasha habari na kutetea kwa elimu ya mtoto wako anapoanza kuingia shule. Maelezo katika Taarifa ya Mpito yanasaidia walimu wa prep waanze kupata kufahamu mtoto wako na kumpanga elimu na mafundisho yanayomfaa. Ikiwa utamtuma mtoto wako kwa *Outside Hours Care (*Utunzaji wa Muda Nje ya Masaa ya Vipindi), Taarifa ya Mpito pia inasaidia watunzaji kupanga kufuatana na mafundisho mengine ya darasani.

Taarifa ya Mpito inayo maelezo ya binafsi pamoja na jina la mtoto wako, tarehe yake ya kuzaliwa, picha, jina lako na anwani yako na namba ya simu. Inawezekana pia kuwa na jina na anwani na namba ya simu ya watunzaji wa watoto wadogo ambao wanahusika na mtoto wako.

Kushirikiana katika kujaza Taarifa ya Mpito ya mtoto wako ni mojawapo ya shughuli ambayo wewe na mtoto wako mweze kufanya pamoja kabla ya shule kuanza na kwa mwaka ufuatao.

### NI SEHEMU GANI YA TRANSITION STATEMENT AMBAYO INANIBIDI NIJAZE?

*Sehemu ya 1 na 1.1* zinajazwa na mtunzaji wa watoto wadogo wa mtoto wako.

*Sehemu ya 1.2*. yaweza kujazwa na mtunzaji wa watoto wachanga wa mtoto wako ikiwa mtoto wako haendelei kama kawaida au amelemaa. Watunzaji wengine wanaohusika katika kumsaidia mtoto wako waweza pia kuleta mawazo yao kwa sehemu hiyo.

*Sehemu ya 2: Mtoto:* inajazwa na mtoto wako kwa kusaidiwa na mtu mzima ambaye amemzoea. Labda ni wewe mwenyewe au mtunzaji au mwalimu wa mtoto wako.

*Sehemu ya 3: Familia:* Wewe unajaza sehemu hii. Ni muhimu ulete mawazo yako unapojaza Taarifa ya Mpito Sehemu hii inayo maswali ambayo yanakusaidia katika kuandika majibu. Kujibu baadhi au yote ya maswali hayo kutawezesha mwalimu wa mtoto wako na mtunzaji wa *Outside Hours Care (*Utunzaji wa Muda Nje ya Masaa ya Vipindi*)* (ikiwa mtoto anasajiliwa hapo) kuwapokea mtoto wako na familia yako vizuri na kutegemeza elimu na maendeleo ya mtoto wako.

### INAKUWAJE BAADA YA MIMI KUJAZA SEHEMU YANGU YA TRANSITION STATEMENT?

Baada ya kujaza *Sehemu ya 3: Familia:* rudisha sehemu hii kwa mwalimu wa sasa wa mtoto wako. Ikiwa umemsaidia mtoto wako kujaza *Sehemu ya 2: Mtoto,* irudishe pamoja na Sehemu ya 3.

Mwalimu wa mtoto wako wa sasa atajumlisha sehemu zote za Taarifa ya Mpito na kukupatia nakala kamili.

Yule mwalimu wa watoto wadogo wa mtoto wako pia atatoa nakala ya Taarifa ya Mpito kamili kwa shule ya

mtoto wako na *Outside School Hours Care (*Utunzaji wa Muda Nje ya Masaa ya Vipindi*)* (ikiwa inahusika).

Ikiwa hujajua ni shule ipi mtoto wako atakayohudhuria, mwalimu wa watoto wachanga wa mtoto wako atakupatia nakala ya pili ya Taarifa ya Mpito ili utoe nakala kwa shule ile ya mtoto wako utakapomsajili.

*Sehemu hii ya 3 Familia,* isipoletwa kwa huduma, halafu mwalimu wa watoto wadogo wa mtoto wako atashirikisha sehemu zingine zilizojazwa tayari kwa shule ya mtoto wako na *Outside School Hours Care (*Utunzaji wa Muda Nje ya Masaa ya Vipindi*)* (ikiwa inahusika) na kukupatia nakala ya yale yaliyoshirikishwa kwako kuitunza.

Utafiti na maoni ya shule yamedokeza kwamba kushirikisha maelezo haya kunategemeza muda huo wa kuanza kuingia shuleni. Hata kama hutaki taarifa kadhaa zinazohusu mtoto wako zishirikishwe na shule ya mtoto wako, tafadhali zungumza na mwalimu wa watoto wadogo wa mtoto wako.

## MAELEZO ZAIDI

Tafadhali nenda kwa
www.education.vic.gov.au/transitiontoschool

Hati hii imetafsiriwa katika lugha mbalimbali ambazo zinapatikana kwenye
www.education.vic.gov.au/transitiontoschool